



TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

JE, WAIJUA



**MISINGI YA USHIRIKA KAMA MIHIMILI NA
MIONGOZO KATIKA
UTEKELEZAJI WA MAADILI YA USHIRIKA**

(I) MSINGI NA. 1

Uanachama wa Hiari na ulio wazi

Vyama vya Ushirika ni vyama vya hiari na uanachama uko wazi kwa watu wote wenye uwezo wa kutumia huduma zake na walio tayari kukubali wajibu na majukumu ya kuwa wanachama bila kubaguliwa kijinsia, kimbari, kijamii, kisiasa au kidini.

(II) MSINGI Na. 2

Wanachama na Udhhibiti wa Kidemokrasia

Vyama vya Ushirika ni vyama vya Kidemokrasia vinavyoongozwa na wanachama wenyewe ambao, kwa vitendo, hushiriki katika malengo yao na kufanya maamuzi. Wale waliochaguliwa kuwa wawakilishi wanawajibika kwa wanachama. Katika vyama vya msingi wanachama wana haki sawa katika kupiga kura (kura moja mtu mmoja) na katika ngazi nyingine Vyama vya Ushirika huendeshwa kwa taratibu za kidemokrasia.

(III) MSINGI Na. 3

Ushiriki wa wanachama katika shughuli za kiuchumi

Wanachama huchangia kwa uwiano wa usawa katika mtaji wa chama chao ambao wanaudhibiti kidemokrasia. Angalau sehemu ya mtaji huo, kwa kawaida huwa ni mali ya jumla ya chama. Kwa kawaida Wanachama hulipwa faida kidogo kama ipo, kutoka katika mtaji uliochangiwa kama sharti la uanachama. Wanachama hutenga ziada kwaajili ya madhumuni yafuatayo:

Kuendeleza chama chao pengine kwa kuweka akiba, ambayo sehemu yake Fulani haigawanywi kuwanufaisha wanachama kwa uwiano wa jinsi walivyoshiriki katika shughuli za chama; na kusaidia katika shughuli zingine kama itakavyokuwa imeidhinishwa na wanachama.

(IV) MSINGI Na. 4

Uhuru na kujitegemea

Vyama vya Ushirika ni vyombo huru na vinavyojitegemea chini ya uongozi na usimamizi wa wanachama.

Iwapo vitaamua kufanya mikataba na vyombo vingine, ikiwemo Serikali au vikiamua kuongeza mtaji kutoka vyanzo vingine vya nje, vyama vitafanya hivyo kwa kuzingatia maamuzi ya wanachama ya kidemokrasia na uhuru wa vyama.

Msingi Na.5


(V) Elimu, mafunzo na taarifa

Vyama vya Ushirika hutoa elimu na mafunzo kwa Wanachama, Halmashauri, Mameneja na Watendaji wengine ili waweze kuchangia inavyopasa katika maendeleo ya vyama vyao. Umma kwa ujumla, huelimishwa hususan vijana na viongozi wahamasishaji, kuhusu ushirika na manufaa yake.

Msingi Na.6

(VI) Ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika

Vyama vya Ushirika hutoa huduma kwa wanachama wake ipasavyo na huimarisha ushirika kwa kushirikiana kwa kutumia miundo iliyopo katika ngazi ya chama cha msingi, Chama Kikuu, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.



Msingi Na.7

(VII) Kuijali Jamii

Vyama vya Ushirika hujihusisha na maendeleo endelevu ya Jamii zake kupitia maamuzi ya wanachama wake.

Kwa maelezo zaidi:

Mrajis wa Vyama vya Ushirika,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC),
S.L.P 201,
DODOMA



Tume ya maendeleo ya Ushirika



Ushirika_tcdc



@ushirika_tcdc

